JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 TOLEO LA MWAKA 2023

2023-2032

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014
# TOLEO LA 2023

**KWA KIPINDI CHA MWAKA 2023 – 2032**

**AGOSTI, 2023**

# YALIYOMO

**YALIYOMO** .......... **2**

**VIFUPISHO** .......... **4**

**MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014, TOLEO LA 2023 KWA KIPINDI CHA MWAKA 2023 – 2032** .......... **5**

1.0 Utangulizi .......... 5

1.1 Hali Ilivyo .......... 6

1.2 Upungufu wa Sera katika Utekelezaji Wake .......... 7

1.3 Changamoto za utoaji wa elimu na mafunzo .......... 7

**2 Dira** .......... **8**

**3 Dhima** .......... **8**

**4 Lengo Kuu** .......... **8**

**5 Malengo Mahsusi** .......... **8**

**6 Mikakati ya Utekelezaji** .......... **9**

6.0 Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu .......... 9

6.1 Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo Nchini .......... 9

6.2 Elimu na Mafunzo yenye Viwango vya Ubora Unaotambulika Kitaifa, Kikanda na Kimataifa .......... 9

6.3 Kuwa na Rasilimaliwatu ya Kutosha na yenye Umahiri na Weledi Stahiki Kuendana na Vipaumbele vya Taifa .......... 10

6.4 Usimamizi na Uendeshaji Madhubuti wa Elimu na Mafunzo .......... 10

6.5 Mfumo Endelevu wa Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo .......... 11

6.6 Mfumo wa Elimu na Mafunzo Unaozingatia Masuala Mtambuka .......... 11

**7 Shabaha** .......... **11**

**7.1 Mfumo, miundo na taratibu nyumbufu** .......... **11**

**7.2 Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo Nchini** .......... **12**

**7.3 Elimu na Mafunzo yenye Viwango vya Ubora Unaotambulika Kitaifa, Kikanda na Kimataifa** .......... **13**

**7.4 Kuwa na Rasilimaliwatu ya Kutosha na Yenye Umahiri na Weledi Stahiki Kuendana na Vipaumbele vya Taifa ........ 15**

**7.5 Usimamizi na Uendeshaji Madhubuti wa Elimu na Mafunzo ........ 16**

**7.6 Mfumo Endelevu wa Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo ........ 17**

**7.7 Mfumo wa Elimu na Mafunzo Unaozingatia Masuala Mtambuka ........ 18**

**8 Mahitaji ya Rasilimali ........ 18**

**9 Muda wa Utekelezaji ........ 19**

**10 Mgawanyo wa Majukumu na Wajibu wa Wadau ........ 19**

10.1 Wizara yenye Dhamana ya Elimu ........ 19
10.2 Wizara yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa za Serikali za Mitaa ........ 19
10.3 Wizara yenye Dhamana ya Fedha ........ 19
10.4 Wizara yenye Dhamana ya Teknolojia ya Habari ........ 20
10.5 Wizara yenye Dhamana ya Ardhi ........ 20
10.6 Wizara yenye Dhamana ya Afya ........ 20
10.7 Wizara yenye Dhamana ya Utamaduni ........ 20
10.8 Wizara yenye Dhamana ya Michezo ........ 20
10.9 Wizara yenye Dhamana ya Utumishi wa Umma ........ 20
10.10 Ofisi yenye Dhamana ya Uandishi wa Sheria ........ 20
10.11 Wizara yenye Dhamana ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ........ 20
10.12 Wizara yenye Dhamana ya Mendeleo ya Mtoto ........ 21
10.13 Wadau wa Maendeleo ........ 21
10.14 Sekta Binafsi ........ 21
10.15 Taasisi za Elimu na Mafunzo ........ 21

**11 Bangokitita la Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ........ 22**

**12 Ufuatiliaji na Tathmini ........ 40**

12.1 Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ........ 40
12.2 Maeneo na Vipengele Muhimu ........ 41

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AZAKI | Asasi za Kiraia |
| HESLB | Higher Education Students' Loans Board |
| KE | Kamishna wa Elimu |
| KM | Katibu Mkuu |
| KMte | Katibu Mtendaji |
| MEF | Mkurugenzi Elimu ya Ufundi |
| MEJ | Mkurugenzi Elimu ya Juu |
| MKUKUTA | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi |
| MMEJU | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu |
| MMES | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari |
| NBS | National Bureau of Statistics |
| ORU | Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma |
| TACAIDS | Tanzania Commission for AIDS |
| TCU | Tanzania Commission for Universities |
| TDMS | Teachers Development and Management Strategy |
| TEA | Tanzania Education Authority |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| VETA | Vocational Education and Training Authority |
| WEMU | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi |
| WKA | Wizara ya Kazi na Ajira |
| WVB | Wizara ya Viwanda na Biashara |

## MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014, TOLEO LA 2023 KWA KIPINDI CHA MWAKA 2023 – 2032

### 1.0 Utangulizi

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023 imeandaliwa kwa madhumuni ya kuwa na wananchi walioelimika, na wenye maarifa na ujuzi ili kuwezesha kuchangia kwa haraka katika maendeleo ya Taifa na kuhimili ushindani. Sera hii imeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ambayo imejielekeza kujenga jamii iliyoelimika na yenye kupenda kujielimisha. Vilevile, imezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Muda Mrefu (2011/12 - 2025/26) ambao umelenga kuboresha maisha ya wananchi.

Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo umeandaliwa kwa lengo la kutafsiri matamko ya Sera na kuwezesha utekelezaji wake. Aidha, Mkakati unaainisha malengo ya Sera, mikakati ya utekelezaji wa malengo hayo, shabaha, viashiria, rasilimali na mgawanyo wa majukumu. Mkakati huu utawezesha kuandaliwa kwa programu ya utekelezaji, itakayowawezesha wadau mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la 2023. Vilevile, mkakati unaongoza asasi na taasisi za elimu na mafunzo nchini kuandaa mipango na programu za utekelezaji wa ajenda ya maendeleo ya elimu kwa muda mrefu, wa kati na mfupi. Mkakati utatekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2023 hadi 2032.

Mambo muhimu yanayotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na kuhuisha Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya uendeshaji wa elimu na mafunzo na kuhuisha miundo na mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote. Masuala mengine ni kuimarisha mifumo ya utawala, usimamizi, ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu na mafunzo; kuinua ubora wa miundombinu ya elimu na mafunzo; kupanua wigo wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote; kuongeza fursa za elimu na mafunzo na kuondoa vikwazo vinavyosababisha wanafunzi kutohitimu katika ngazi mbalimbali; na kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera ya Elimu na Mafunzo. Aidha, matumizi ya Lugha ya Kiswahili, Kiingereza, Lugha ya Alama ya Tanzania, Lugha ya Mguso na Breli pamoja na lugha nyingine za kigeni katika elimu na mafunzo yataimarishwa.

Matokeo chanya yanayotarajiwa kupatikana baada ya mkakati kutekelezwa ni pamoja na: kuwa na wastani wa asilimia 12 ya Watanzania wenye ujuzi wa juu; asilimia 33

wenye ujuzi wa kati na asilimia 55 wenye ujuzi wa chini. Vilevile, kuwa na asilimia 94 ya vijana kati ya umri wa miaka 15 na 24 wenye kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Aidha, asilimia 95 ya wanafunzi wa rika lengwa kuhitimu Elimu ya lazima ya hadi kidato cha Nne; kuimarisha uwiano kati ya mwalimu kwa wanafunzi kufikia 1:45 kwa Elimu ya msingi, kuimarisha upatikanaji wa walimu kwa elimu ya sekondari kwa kuzingatia masomo ya kila ngazi na kuongeza udahili wa wanafunzi katika elimu ya juu na kuimarisha upatikanaji wa wahadhiri mahiri.

## 1.1 Hali Ilivyo

Katika kutekeleza malengo yaliyowekwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, elimu ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa nguzo muhimu za dira. Elimu katika Dira inatazamwa si tu kama nyenzo muhimu ya kufikia malengo ya Dira, bali elimu yenyewe ni sehemu ya malengo mahsusi ya Dira. Dira ya Maendeleo ya Taifa inalenga, pamoja na mambo mengine, kuiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati shindani. Ili kufanikisha azma hiyo, limewekwa lengo mahsusi la kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2025, Tanzania inakuwa na jamii iliyoelimika na inayopenda kujielimisha zaidi.

Katika kutambua umuhimu wa elimu ili kufikia malengo yaliyomo katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Sekta ya Elimu imekuwa ikipewa kipaumbele. Kwa mfano, katika Bajeti ya Taifa ya mwaka 2019/20, ilitengewa asilimia 17.9, mwaka 2020/21 ilitengewa asilimia 18.0 na mwaka 2021/22 ilitengewa asilimia 18.9, ikiwa ni kati ya sekta zinazotengewa bajeti kubwa. Katika kufanikisha malengo ya elimu, Serikali imekuwa ikitekeleza Sera, mipango, miongozo na mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Sera ya Elimu ya Msingi na Sekondari bila Ada; Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP), Mkakati wa Elimu Jumuishi; na Mwongozo wa Kurudisha Shule Wanafunzi walioacha masomo kwa sababu mbalimbali.

Mafanikio mbalimbali yamepatikana katika utekelezaji wa mipango hiyo. Mafanikio hayo ni pamoja na: kuongezeka kwa uandikishaji katika Elimu ya Awali kutoka 1,069,823 mwaka 2015 hadi 1,543,843 mwaka 2022; Elimu ya Msingi kutoka 8,298,282 mwaka 2015 hadi 11,420,973 mwaka 2022, Elimu ya Sekondari ya Chini kutoka 1,675,593 mwaka 2016 hadi 2,645,115 mwaka 2022; Sekondari ya Juu kutoka 131,362 mwaka 2016 hadi 178,473 mwaka 2022; Mafunzo ya Ufundi Stadi kutoka 119,184 mwaka 2017/18 hadi 380,748 mwaka 2021; Elimu ya Ufundi kutoka 128,940 mwaka 2017/18 hadi 179,518 mwaka 2021/22; Vyuo Vikuu kutoka 225,330 mwaka 2015/16 hadi 240,523 mwaka 2022/23. Kuimarika kwa huduma mbalimbali katika taasisi za elimu na mafunzo ambapo hadi mwaka 2022 idadi ya shule zilizounganishwa katika umeme wa gridi ya Taifa ni shule za msingi 10,793 kati ya 19,261 na 4,276 kati ya shule 5,540 za sekondari. Pia, huduma za ushauri na unasihi zimeimarika ambapo kila taasisi ya elimu na mafunzo ina idara au kitengo cha

huduma za ushauri nasaha kuwahudumia wanafunzi na wafanyakazi. Mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa elimu na mafunzo nchini hivyo kuchangia uandikishaji wa rika lengwa katika elimu ya msingi kutoka asilimia 85.8 na asilimia 33.4 mwaka 2016 kufikia asilimia 87 mwaka 2022 na sekondari (Kidato cha 1-4) asilimia 38.3 mwaka 2022 mtawalia; kuimarika kwa usimamizi wa utumishi wa walimu; kuongezeka kwa wanufaika wa mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka wanafunzi 53,802 mwaka 2015/16 hadi 202,877 na kuanzishwa kwa SAMIA *Scholarship* mwaka 2022/23 ambapo wanafunzi 636 wamenufaika; na kuongeza ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika taasisi za elimu na mafunzo kwa ngazi zote.

## 1.2 Upungufu wa Sera katika Utekelezaji Wake

Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ina upungufu katika baadhi ya maeneo ambapo Sera haikuweza kutoa ufafanuzi wa kutosha hivyo kutoa mwanya wa tafsiri tofauti katika baadhi ya maeneo ya msingi kama vile; muundo wa elimu; ujuzi uliokusudiwa na lugha ya kufundishia, umri wa kuanza elimu ya awali na elimu ya msingi kutokuwa mahsusi. Pia, baadhi ya maeneo ya Sera hayakutekelezwa kama: mfumo wa elimu ya lazima wa miaka kumi; kutokuwepo kwa Sheria ya elimumsingi na sekondari; kukosekana kwa utaratibu wa kuwezesha maendeleo ya wanafunzi wenye vipaji, vipawa na kasi tofauti na mahitaji maalum; na kukosekana kwa utaratibu na utambuzi wa maarifa, ujuzi na stadi zilizopatikana nje ya mfumo wa shule. Aidha, Sera pia haikuzingatia baadhi ya maeneo yakiwemo elimu ya ualimu, elimu ya juu, utafiti katika elimu na ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa elimu na mafunzo; malengo ya jumla ya Elimu na kwa kila ngazi ya elimu na mafunzo. Upungufu huo umeweka msukumo wa kuandaa toleo jipya la Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023 linalorekebisha upungufu uliobainishwa.

## 1.3 Changamoto za utoaji wa elimu na mafunzo

Jukumu kuu la sekta ya elimu ni kuzalisha nguvukazi ya kutosha na yenye umahiri na weledi stahiki katika ngazi mbalimbali na katika uwiano stahiki kwa maendeleo ya Taifa. Katika jitihada za kutekeleza jukumu hilo, sekta inakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwemo: mfumo wa elimu kujikita zaidi kwenye elimu ya jumla na kukosa fursa anuai za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji, njia mbalimbali za ujifunzaji kulingana na mazingira; mitaala katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia; mfumo usio fanisi wa uthibiti na ithibati ya elimu na mafunzo katika ngazi zote; upungufu wa nguvukazi ya kutosha yenye maarifa, stadi na ujuzi unaohitajika kwa ajili ya sekta mbalimbali; mfumo usio fanisi wa

usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo; mfumo usio wa uhakika na endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo wenye vyanzo anuai na endelevu; na kutozingatiwa kwa masuala yanayoibuka ambayo yanaathiri utoaji wa elimu na mafunzo.

## 2 Dira

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika, mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaomwezesha kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa.

## 3 Dhima

Kuinua ubora wa elimu na mafunzo kwa kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika, wenye stadi na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa.

## 4 Lengo Kuu

Kuwa na mfumo wa elimu na mafunzo wenye kumuandaa Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaomwezesha kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa.

## 5 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya Sera ni kuwa na:

(i) Mfumo, muundo na taratibu nyumbufu kumwezesha kila Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali kitaaluma na kitaalamu;

(ii) Fursa mbalimbali za elimu na mafunzo nchini;

(iii) Elimu na mafunzo yenye viwango vya ubora unaotambulika kitaifa, kikanda na kimataifa;

(iv) Rasilimaliwatu ya kutosha na yenye umahiri na weledi stahiki kuendana na vipaumbele vya Taifa;

(v) Usimamizi na uendeshaji madhubuti wa elimu na mafunzo nchini;

(vi) Mfumo endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo nchini; na

(vii) Mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia masuala mtambuka.

## 6 Mikakati ya Utekelezaji

Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 itatekelezwa kupitia mikakati mbalimbali ambayo imeainishwa kuendana na malengo mahsusi ya Sera kama ifuatavyo:

### 6.0 Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu

(i) Kuimarisha mfumo wa elimu na mafunzo ili utoe fursa anuai za kumwezesha mhitimu kupata ujuzi, maarifa na stadi kwa ajili ya ulimwengu wa kazi kulingana na uwezo, matakwa na malengo yake.

(ii) Kuimarisha utoaji wa elimu ya lazima kwa muda wa miaka kumi.

(iii) Kuimarisha mifumo ya mitaala, upimaji na tathmini na tuzo kwa ngazi zote za elimu na mafunzo.

### 6.1 Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo Nchini

(i) Kuimarisha ushiriki wa makundi mbalimbali ya kijamii katika kupata elimu na mafunzo katika ngazi zote.

(ii) Kuimarisha utaratibu wa utambuzi wa vipaji na vipawa katika ngazi mbalimbali na kuviendeleza.

(iii) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu.

(iv) Kuimarisha utaratibu wa utambuzi wa ujuzi na maarifa yaliyopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo.

(v) Kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya watu wazima na ujifunzaji endelevu.

### 6.2 Elimu na Mafunzo yenye Viwango vya Ubora Unaotambulika Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

(i) Kuimarisha usimamizi, ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.

(ii) Kuimarisha mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote ili ikidhi mahitaji ya ulimwengu wa kazi katika kuleta maendeleo ya Taifa.

(iii) Kuimarisha utoaji wa elimu ya ualimu ili kuandaa walimu kutekeleza kwa ufanisi mitaala ya ujenzi wa umahiri na kukuza stadi za karne ya 21.

(iv) Kuimarisha uandaaji na usambazaji wa nyenzo, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia.

(v) Kuimarisha miundombinu na upatikanaji wa samani bora, toshelevu na rafiki katika taasisi za elimu na mafunzo.

(vi) Kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika elimu na mafunzo.

(vii) Kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha mbalimbali katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

(viii) Kuimarisha umahiri wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika kufundishia ngazi zote za elimu na mafunzo.

### 6.3 Kuwa na Rasilimaliwatu ya Kutosha na yenye Umahiri na Weledi Stahiki Kuendana na Vipaumbele vya Taifa

(i) Kuimarisha upatikanaji wa rasilimaliwatu kwa ajili ya sekta ya elimu kulingana na vipaumbele vya Taifa.

(ii) Kuimarisha usimamizi wa usajili, viwango na maadili katika taaluma ya ualimu kwa sekta ya umma na binafsi.

(iii) Kuimarisha upatikanaji wa rasilimaliwatu kwa ajili ya sekta nyingine kulingana na vipaumbele vya Taifa.

### 6.4 Usimamizi na Uendeshaji Madhubuti wa Elimu na Mafunzo

(i) Kuimarisha uongozi, usimamizi na uendeshaji ili uwe fanisi katika sekta ya elimu.

(ii) Kuimarisha ushirikiano katika masuala ya elimu na mafunzo baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.

(iii) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa takwimu za elimu na mafunzo nchini.

(iv) Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika ya elimu na mafunzo.

(v) Kuimarisha upatikanaji, urasimishaji na matumizi fanisi ya ardhi kwa ajili ya utoaji wa elimu na mafunzo.

### 6.5 Mfumo Endelevu wa Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo

(i) Kuimarisha mfumo wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.

(ii) Kuimairisha ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika ugharimiaji wa elimu na mafunzo.

### 6.6 Mfumo wa Elimu na Mafunzo Unaozingatia Masuala Mtambuka

(i) Kuimarisha masuala mtambuka katika utoaji wa elimu na mafunzo.

(ii) Kuimarisha uwezo wa taasisi za elimu na mafunzo katika kukabiliana na dharura zinazoathiri utoaji wa elimu na mafunzo.

(iii) Kuimarisha uwezo wa taasisi za elimu na mafunzo kufanya utafiti na kuchapisha matokeo kwenye majarida yenye hadhi ya kimataifa.

## 7 Shabaha

Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 itatekelezwa kulenga shabaha mbalimbali ambazo zimeainishwa kuendana na malengo mahsusi ya Sera kama ifuatavyo:

### 7.1 Mfumo, miundo na taratibu nyumbufu

(i) Mikondo ya elimu ya amali na elimu ya jumla kuanzishwa ifikapo Januari, 2028;

(ii) Njia huria na masafa na changamani kutumika katika utoaji wa elimu na mafunzo katika shule na Vyuo ifikapo Juni, 2025;

(iii) Utaratibu wa kutambua sifa zinazopatikana nje ya mfumo rasmi na mikondo tofauti kulingana na mfumo wa Taifa wa Tuzo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(iv) Elimu ya lazima ya miaka kumi kuidhinishwa ifikapo Desemba, 2023;

(v) Miongozo ya utoaji wa elimu na mafunzo ya lazima kuhuishwa ifikapo Juni, 2024;

(vi) Elimu kwa umma kuhusu Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera kutolewa ifikapo Juni, 2028;

(vii) Mfumo wa Taifa wa Mitaala kuhuishwa ifikapo Juni, 2025;

(viii) Mfumo wa Taifa wa upimaji na tathmini kuhuishwa ifikapo Juni, 2025; na

(ix) Mfumo wa Taifa wa Sifa Linganifu na Tuzo kuhuishwa ifikapo Juni, 2025.

### 7.2 Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo Nchini

(i) Miundombinu toshelevu kwa utoaji wa elimu ya lazima kuandaliwa ifikapo Juni, 2032;

(ii) Miundombinu toshelevu kwa utoaji wa elimu ya amali kwa sekondari ngazi ya chini kuandaliwa ifikapo Juni, 2032;

(iii) Mwongozo wa utoaji elimu jumuishi kuhuishwa ifikapo Juni, 2025;

(iv) Kuweka mazingira wezeshi kwa wasichana kujiunga na elimu ya amali na elimu ya juu hususani masomo ya sayansi, teknolojia na Hisabati ifikapo Juni, 2025;

(v) Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza kutoka elimu ya msingi kufikia asilimia 100 ifikapo Juni, 2025;

(vi) Kuhuisha programu za elimu na mafunzo kwa walioikosa ifikapo Juni, 2025;

(vii) Mwongozo wa kubaini na kuendeleza vipaji na vipawa katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(viii) Kubaini taasisi mahsusi kwa ajili ya kuendeleza wanafunzi wenye vipawa na vipaji katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo ifikapo Juni, 2026;

(ix) Miundombinu muhimu ya teknolojia katika utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote kuandaliwa ifikapo Juni, 2032;

(x) Vifaa vya TEHAMA kusambazwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo ifikapo Juni, 2032;

(xi) Mfumo wa ushirikiano baina ya Serikali na wadau wa elimu katika uwekezaji katika teknolojia kwa ajili ya utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote kuandaliwa na kutumika ifikapo Juni 2025;

(xii) Mwongozo wa utambuzi wa ujuzi na maarifa yaliyopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo kuhuishwa ifikapo Juni, 2024;

(xiii) Programu za utambuzi na uendelezaji wa ujuzi na maarifa yaliyopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo kuanzishwa ifikapo Juni, 2025;

(xiv) Programu mbalimbali za elimu ya watu wazima na kisomo chenye manufaa kuhuishwa ifikapo Juni, 2025; na

(xv) Programu mbalimbali za elimu isiyo na ukomo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025.

### 7.3 Elimu na Mafunzo yenye Viwango vya Ubora Unaotambulika Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

(i) Mwongozo wa usimamizi, ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu katika ngazi zote kuhuishwa ifikapo Juni, 2024;

(ii) Usimamizi, ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu kushirikisha wadau ifikapo Juni 2025;

(iii) Elimu ya amali kujumuishwa katika mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote ifikapo Juni, 2024;

(iv) Programu za Elimu ya amali baada ya ngazi ya tatu (NVA 3) kuanzishwa ifikapo Juni, 2025;

(v) Stadi za karne ya 21 kujumuishwa katika mitaala ya ngazi zote ifikapo Juni, 2024;

(vi) Vigezo vya ulinganifu baina ya programu zinazofanana katika taasisi mbalimbali kuhuishwa ili kujumuisha mahiri za ulimwengu wa kazi ifikapo Juni, 2025;

(vii) Mitaala ya Sayansi, Hisabati na Teknolojia kuhuishwa ifikapo Juni, 2025;

(viii) Utaratibu wa utoaji wa mafunzo kwa nadharia na vitendo kwa kushirikiana na viwanda, mashamba na taasisi za huduma kuanzishwa ifikapo Juni, 2026;

(ix) Mfumo wa upimaji na tathmini ya mitaala kwa kuzingatia mahiri zinazohitajika kwa kila ngazi kuhuishwa ifikapo Juni, 2025;

(x) Mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote kujumuisha stadi za kujenga uzalendo, amani na maadili ifikapo Juni 2024;

(xi) Elimu ya ualimu wa mafunzo ya amali kujumuishwa katika mitaala ya elimu ya ualimu ifikapo Juni, 2024;

(xii) Mbinu za ufundishaji wa Stadi za karne ya 21 kujumuishwa katika mitaala ya elimu ya ualimu ifikapo Juni, 2024;

(xiii) Vigezo vya kujiunga na elimu ya ualimu kwa ngazi mbalimbali kuhuishwa ifikapo Juni, 2025;

(xiv) Programu za mafunzo kwa walimu tarajali chini ya uangalizi (internship) kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo Juni, 2026;

(xv) Umahiri wa masuala ya ushauri na unasihi kujumuishwa katika programu za elimu ya ualimu katika ngazi zote ifikapo Juni, 2024;

(xvi) Mfumo wa uandaaji na usambazaji wa nyenzo, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia kuhuishwa ifikapo Juni, 2025;

(xvii) Nyenzo, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia kuandaliwa kulingana na mahitaji ifikapo Juni, 2032;

(xviii) Nyenzo, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia kusambazwa kulingana na mahitaji ifikapo Juni, 2032;

(xix) Huduma za maktaba na njia mbadala za upatikanaji wa maarifa katika jamii, na taasisi za elimu na mafunzo kuimarishwa ifikapo Juni, 2027;

(xx) Utaratibu wa ushirikiano baina ya Serikali na wadau wa ndani na nje na mashirika ya kimataifa katika kubadilishana uzoefu na teknolojia ya huduma za maktaba kuandaliwa ifikapo Juni, 2026;

(xxi) Utaratibu wa matumizi na utunzaji wa miundombinu ya elimu na mafunzo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(xxii) Wadau kushirikishwa katika upatikanaji wa miundombinu na samani ifikapo Juni, 2025;

(xxiii) Mwongozo wa Taifa wa dawati la ulinzi na usalama wa mtoto ndani na nje ya shule kuhuishwa ifikapo Juni, 2024;

(xxiv) Mwongozo wa chakula na lishe katika ngazi za elimu na mafunzo kuhuishwa ifikapo Juni, 2024;

(xxv) Mwongozo wa malezi, ushauri na unasihi na ulinzi wa mwanafunzi wa shule na vyuo kuhuishwa ifikapo Julai, 2024;

(xxvi) Mwongozo wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kwa ngazi mbalimbali kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(xxvii) Vifaa na maabara za lugha katika taasisi za elimu na mafunzo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(xxviii) Programu za kuendeleza Lugha ya Alama ya Tanzania, Lugha ya Alama Mguso na Breli kuandaliwa ifikapo Juni, 2026;

(xxix) Mwongozo wa Matumizi ya Lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo kuandaliwa ifikapo Desemba, 2024; na

(xxx) Programu za kujenga umahiri wa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza kuandaliwa ifikapo Juni, 2025.

### 7.4 Kuwa na Rasilimaliwatu ya Kutosha na Yenye Umahiri na Weledi Stahiki Kuendana na Vipaumbele vya Taifa

(i) Mahitaji ya walimu, wakufunzi na wanataaluma kubainishwa ifikapo Juni, 2024;

(ii) Mwongozo wa upatikanaji wa walimu, wakufunzi na wanataaluma tarajali kuandaliwa ifikapo Juni, 2026;

(iii) Walimu, wakufunzi na wanataaluma mahiri kuandaliwa kulingana na mahitaji ifikapo Juni, 2032;

(iv) Mwongozo wa kitaifa wa mgawanyo wa walimu, wakufunzi na wanataaluma kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(v) Mwongozo wa kuwabakiza kazini walimu, wakufunzi na wanataaluma kuandaliwa ifikapo Juni, 2026;

(vi) Mahitaji ya ajira kwa ajili ya sekta ya elimu kubainishwa ifikapo Juni, 2032;

(vii) Utaratibu wa ajira za wanataaluma wabobezi kutoka nje ya nchi kuhuishwa ifikapo Juni, 2026;

(viii) Usajili na viwango vya taaluma ya ualimu katika sekta ya umma na binafsi kusimamiwa na chombo kimoja chini ya wizara yenye dhamana ya elimu ifikapo Juni, 2026;

(ix) Programu za mafunzo kazini kwa walimu, wakufunzi na wanataaluma kuhuishwa ifikapo Juni, 2026;

(x) Mfumo na taratibu za usimamizi, ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu ya ualimu kuhuishwa ifikapo Juni 2025;

(xi) Tathmini ya mahitaji halisi ya ujuzi kwa ajili ya sekta nyingine kufanyika ifikapo Juni, 2025;

(xii) Rasilimaliwatu kulingana na mahitaji ya Taifa kuandaliwa ifikapo 2032; na

(xiii) Mwongozo wa kitaifa wa utambuzi wa ujuzi kuandaliwa ifikapo Juni, 2026.

## 7.5 Usimamizi na Uendeshaji Madhubuti wa Elimu na Mafunzo

(i) Mwongozo wa kuwapata viongozi katika sekta ya elimu kuhuishwa ifikapo Juni, 2025;

(ii) Mfumo wa sheria za elimu na mafunzo kuhuishwa ifikapo Juni, 2024;

(iii) Majukumu ya vyombo mbalimbali vya uongozi na usimamizi wa elimu na mafunzo kuhuishwa ifikapo Juni, 2026;

(iv) Matokeo na matumizi ya tafiti zinazofanyika katika sekta ya elimu kuzingatiwa katika maamuzi ifikapo Juni, 2026;

(v) Mwongozo wa kuendeleza ushirikiano katika elimu baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhuishwa ifikapo Juni, 2025;

(vi) Hati za makubaliano katika elimu na mafunzo baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhuishwa ifikapo Juni, 2025;

(vii) Mfumo unganifu wa ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa takwimu za elimu na mafunzo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(viii) Rasilimaliwatu yenye uwezo wa kukusanya, kuchakata, kuhakiki, na kuhifadhi takwimu za elimu na mafunzo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(ix) Utaratibu wa usimamizi wa mikataba ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(x) Mpango wa utekelezaji wa mikataba ya ushirikiano katika elimu na mafunzo kikanda na kimataifa kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(xi) Mipango ya upatikanaji na urasimishaji wa ardhi kwa ajili ya taasisi za elimu na mafunzo kuandaliwa na kutumika ifikapo Juni, 2025; na

(xii) Mipango endelevu na fanisi ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya taasisi za elimu na mafunzo kuandaliwa na kutumika ifikapo Juni, 2025.

### 7.6 Mfumo Endelevu wa Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo

(i) Vyanzo anuai/mbadala na endelevu vya kugharimia elimu na mafunzo katika ngazi zote kubainishwa ifikapo Juni 2026;

(ii) Miongozo ya mikopo, ada, ruzuku, michango, ufadhili wa masomo katika ngazi zote za elimu na mafunzo kuhuishwa ifikapo Desemba, 2024;

(iii) Gharama halisi za kumsomesha mwanafunzi kwa kila ngazi ya elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji kukokotolewa ifikapo Juni, 2024; na

(iv) Programu za ushirikishwaji wa wadau katika kugharimia elimu na mafunzo kuandaliwa na kutumika ifikapo Juni, 2024.

### 7.7 Mfumo wa Elimu na Mafunzo Unaozingatia Masuala Mtambuka

(i) Maudhui ya mazingira, magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza kubainishwa na kuchopekwa katika mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote ifikapo Juni, 2024;

(ii) Mwongozo wa shughuli za mtaala nje ya darasa katika ngazi zote kuhuishwa na kutumika ifikapo Juni, 2024;

(iii) Mwongozo wa kukabiliana na dharura zinazoathiri utoaji wa elimu na mafunzo kuhuishwa na kutumika ifikapo Juni, 2024;

(iv) Taasisi za elimu na mafunzo kuwezeshwa katika kukabiliana na majanga ifikapo Juni, 2025;

(v) Mwongozo wa utafiti na uchapishaji wa matokeo katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025;

(vi) Programu za kuwezesha taasisi za elimu na mafunzo kufanya utafiti kulingana na vipaumbele vya taifa katika ngazi zote za elimu na mafunzo kuandaliwa ifikapo Juni, 2025; na

(vii) Jukwaa la elimu linalohusisha watafiti na wadau kuanzishwa na kuanza kufanya kazi ifikapo Juni, 2025.

## 8 Mahitaji ya Rasilimali

Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023, utatekelezwa kwa kipindi cha miaka 10, kuanzia mwaka 2024 hadi 2033. Utekelezaji wake unakadiriwa kugharimu jumla ya SH 18,435,452,428,864 kutoka bajeti kuu ya Serikali, Sekta binafsi, jamii, na Wadau wa Maendeleo. Makadirio ya kina yameoneshwa katika bangokitita la mkakati wa utekelezaji wa Sera.

Mafanikio ya utekelezaji wa Mkakati yatahusisha shughuli mbalimbali, muda na rasilimali ambazo ni adimu. Hivyo, vyanzo vipya na anuai vitabuniwa kwa ajili ugharimiaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ambavyo vitaiwezesha Wizara yenye

dhamana ya elimu kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kushirikiana na wadau wengine.

Kwa mantiki hiyo, Wizara yenye dhamana ya elimu itaandaa Mkakati wa Utafutaji wa Rasilimali kuendana na malengo, vipaumbele na matarajio ya utekelezaji wa Mkakati. Mkakati huu utasaidia kuongeza wigo wa upatikanaji endelevu wa rasilimali.

## 9 Muda wa Utekelezaji

Mkakati utatekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2023 hadi mwaka 2032. Mkakati utafanyiwa tathmini ya muda wa kati na mwaka wa mwisho wa utekelezaji.

## 10 Mgawanyo wa Majukumu na Wajibu wa Wadau

Ili kutekeleza mkakati huu, inatarajiwa kuwa wadau wakuu watashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa malengo, mikakati na shabaha zilizoainishwa. Wadau wakuu wa utekelezaji wa mkakati huu na majukumu yao ni kama ifuatavyo:

### 10.1 Wizara yenye Dhamana ya Elimu

Wizara yenye dhamana ya elimu itakuwa na majukumu ya kuratibu utekelezaji wa mkakati ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mkakati, mipango, na programu mbalimbali za uendelezaji wa Sera; mapitio ya sheria, kanuni, na miongozo iliyopo kwa muda wa kati na tamati; maandalizi ya miongozo mipya na elimu kwa umma.

### 10.2 Wizara yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa za Serikali za Mitaa

Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itakuwa na jukumu la kuunganisha Serikali kuu na jamii katika utekelezaji wa mkakati huu katika ngazi za mkoa, halmashauri, kata, na shule/chuo.

### 10.3 Wizara yenye Dhamana ya Fedha

Wizara yenye dhamana ya fedha itakuwa na jukumu la kuwezesha upatikanaji wa rasilimalifedha kwa ajili ya ugharimiaji wa mkakati huu katika ngazi zote. Aidha, itahusika na utoaji wa sera za jumla za kiuchumi, miongozo na mipango ya fedha na takwimu.

### 10.4 Wizara yenye Dhamana ya Teknolojia ya Habari

Wizara yenye dhamana ya teknolojia ya habari itakuwa na jukumu la utekekezaji wa mkakati kwa kutoa miongozo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), uendelezaji wa mifumo ya TEHAMA na usalama wa mifumo ya TEHAMA.

### 10.5 Wizara yenye Dhamana ya Ardhi

Wizara yenye dhamana ya Ardhi itakuwa na jukumu la utekelezaji wa Mkakati kwa kutoa Miongozo ya maendeleo ya ardhi kwa shughuli za elimu na mafunzo; uthamini wa ardhi na hatimiliki za ardhi kwa maendeleo ya elimu na mafunzo nchini.

### 10.6 Wizara yenye Dhamana ya Afya

Wizara yenye dhamana ya Afya itakuwa na jukumu la ukaguzi wa huduma za afya na kutoa miongozo kuhusu kinga na tiba, chakula na lishe itakayozingatiwa na taasisi za elimu na mafunzo.

### 10.7 Wizara yenye Dhamana ya Utamaduni

Wizara yenye dhamana ya utamaduni itakuwa na jukumu la kutoa miongozo kuhusu uhamasishaji na uendelezaji wa utamaduni katika taasisi za elimu na mafunzo.

### 10.8 Wizara yenye Dhamana ya Michezo

Wizara yenye dhamana ya michezo itakuwa na jukumu la kutoa miongozo kuhusu uhamasishaji na uendelezaji wa michezo katika taasisi za elimu na mafunzo.

### 10.9 Wizara yenye Dhamana ya Utumishi wa Umma

Wizara yenye dhamana ya utumishi wa umma itakuwa na jukumu la kutoa miongozo kuhusu utawala wa utumishi wa umma, mikataba ya utendaji kazi, maslahi na mipango ya maendeleo ya rasilimali watu na maadili ya utumishi wa umma katika sekta ya elimu.

### 10.10 Ofisi yenye Dhamana ya Uandishi wa Sheria

Ofisi yenye dhamana ya uandishi wa sheria itakuwa na jukumu la kutekeleza mkakati kwa kuandika sheria mpya au/na kurekebisha sheria zilizopo ili kuwezesha utekelezaji wa Mkakati.

### 10.11 Wizara yenye Dhamana ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

Wizara yenye dhamana ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa itakuwa na jukumu la utekelezaji wa mkakati kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya elimu katika kuandaa, kuhuisha na kutekeleza mikataba na itifaki mbalimbali za kuwezesha

uimarishaji wa ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya elimu na mafunzo.

### 10.12 Wizara yenye Dhamana ya Mendeleo ya Mtoto

Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya mtoto itakuwa na jukumu la kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya elimu katika uwianishaji wa malezi na makuzi ya mtoto yatolewayo katika vituo vya kulelea watoto na elimu ya awali.

### 10.13 Wadau wa Maendeleo

Wadau wa Maendeleo watahusishwa katika kutafuta rasilimali za kuwezesha utekelezaji wa mkakati kwa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo.

### 10.14 Sekta Binafsi

Sekta Binafsi watakuwa na jukumu la kutekeleza mkakati kwa kushiriki katika ujenzi wa shule na Vyuo, kuchangia katika ujenzi wa miundombinu, uzalishaji wa nyenzo, zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

### 10.15 Taasisi za Elimu na Mafunzo

Taasisi za Elimu na Mafunzo ikiwemo shule na vyuo zitakuwa na jukumu la kutekeleza mkakati katika maeneo yao. Aidha, watashirikisha jamii katika kutekeleza shughuli mbalimbali katika maeneo yao kwa kuzingatia maelekezo ya Sera. Taasisi za elimu na mafunzo zitawajibika pia kutoa taarifa za utekelezaji wa mkakati katika maeneo yao kwa mamlaka husika.

## 12 Ufuatiliaji na Tathmini

Utekelezaji wa Mkakati wa Sera unahitaji ufuatiliaji na tathmini ili kutoa taarifa ya kufikiwa kwa malengo ya Sera. Lengo kuu la Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ni kutoa mwongozo wa utekelezaji wa Mkakati wa Sera ili kuleta utekelezaji wenye tija na fanisi. Malengo mahsusi ya Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ni:



i. Kuweka shabaha na viashiria vya upimaji wa maendeleo ya utekelezaji wa Sera;

ii. Kutoa mwongozo wa ushiriki wa wadau katika utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini

## 11 Bangokitita la Mkakati wa Utekelezaji wa Sera

| **1. Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lengo | **Mkakati** | **Shabaha** | **Viashiria** | **Rasilimali** | **Muda** | **Mhusika** |
| **A. Utekelezaji wa Sera ya Elimu katika maeneo yasiyokuwa na mabadiliko** | | | | | | |
| Utekelezaji wa afua za Sekta ya elimu kwa kuzingatia tengeo la sasa | | | | 51,800,000,000,000.00 | Julai 2024-Juni 2033 | Sekta ya Elimu |
| **B. Utekelezaji wa Sera ya Elimu katika maeneo yenye msukumo mpya** | | | | | | |
| 3.1 Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu Kumwezesha Mtanzania Kujiendeleza kwa Njia Mbalimbali katika mikondo ya kitaaluma na kitaalamu | Kuimarisha mfumo wa elimu na mafunzo ili utoe fursa anuai za kumwezesha mhitimu kupata ujuzi, maarifa na stadi kwa ajili ya ulimwengu wa kazi kulingana na uwezo matakwa na malengo yake. | Mikondo ya elimu ya amali na elimu ya jumla kuanzishwa ifikapo Januari, 2024 | Idadi ya mikondo iliyoanzishwa | 219,720,000.00 | Julai 2024-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi. |
| | | Njia huria na masafa na changamani kutumika katika utoaji wa elimu na mafunzo katika shule na Vyuo ifikapo Juni, 2025 | Idadi ya shule na Vyuo vinavyotumia njia huria na masafa na changamani | 261,500,000.00 | Julai 2024-Juni 2025 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara yenye dhamana ya Teknolojia, Sekta binafsi. |
| | | Utaratibu wa kutambua sifa zinazopatikana nje ya mfumo rasmi na mikondo tofauti kulingana na mfumo wa Taifa wa Tuzo kuandaliwa ifikapo Juni, | Mwongozo wa utambuzi wa sifa | 5,485,543,861.44 | Julai 2024-Juni-2029 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi, na taasisi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2029 | | | | za elimu na mafunzo. |
| | Kuimarisha utoaji wa elimu ya lazima kwa muda wa miaka kumi | Elimu ya lazima ya miaka kumi kuidhinishwa ifikapo Desemba, 2023 | Elimu ya lazima kuidhinishwa | 234,600,000.00 | Oktoba 2023-Desemba 2023 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi. |
| | | Miongozo ya utoaji wa elimu na mafunzo ya lazima kuhuishwa ifikapo Juni, 2024 | Idadi ya miongozo iliyohuishwa | 48,000,000.00 | Oktoba 2023-Juni 2024 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI. |
| | | Elimu kwa umma kuhusu Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera kutolewa ifikapo Juni, 2028 | Idadi ya programu za uelewa kwa umma kuhusu Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera | 2,034,665,962.50 | Julai 2024-Juni 2028 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi. |
| | Kuimarisha mifumo ya mitaala, upimaji na tathmini na tuzo kwa ngazi zote za elimu na mafunzo. | Mfumo wa Taifa wa Mitaala kuhuishwa ifikapo Juni, 2025 | Idadi ya mifumo ya mitaala iliyohuishwa | 544,300,000.00 | Julai 2024-Juni 2025 | Wizara yenye dhamana ya elimu, na Taasisi za elimu na mafunzo. |
| | | Mfumo wa taifa wa upimaji na tathmini kuhuishwa ifikapo Juni, 2025 | Idadi ya mifumo ya upimaji na tathmini iliyohuishwa | 655,500,000.00 | Julai 2024-Juni 2025 | Wizara yenye dhamana ya elimu, na Taasisi za elimu na mafunzo. |
| | | Mfumo wa Taifa wa Sifa Linganifu na Tuzo kuhuishwa ifikapo Juni, 2027 | Idadi ya mifumo ya sifa linganifu na tuzo iliyohuishwa. | 1,528,500,000.00 | Julai 2024-Juni 2027 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi. |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| **Jumla ya Lengo** | | | | **11,012,329,823.94** | | |
| **2.** Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo | | | | | | |
| **Lengo** | **Mkakati** | **Shabaha** | **Viashiria** | **Rasilimali** | **Muda** | **Mhusika** |
| 3.2 Kuwa na fursa mbalimbali za elimu na mafunzo nchini | Kuimarisha ushiriki wa makundi mbalimbali ya kijamii katika kupata elimu na mafunzo katika ngazi zote | Miundombinu toshelevu kwa utoaji wa elimu ya lazima kuandaliwa ifikapo Juni, 2032 | Kuimarika kwa uwiano wa darasa, matundu ya vyoo, maabara, maktaba, karakana kwa wanafunzi. | 9,080,192,844,651.96 | Oktoba 2023-Juni 2032 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya fedha, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za elimu na mafunzo, Wadau wa Maendeleo, Sekta binafsi. |
| | | Miundombinu toshelevu kwa utoaji wa elimu ya amali kwa sekondari ngazi ya chini kuandaliwa ifikapo Juni, 2032 | Kuimarika kwa uwiano wa maabara na karakana kwa wanafunzi | 1,818,690,028,431.17 | Oktoba 2023-Juni 2032 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya fedha, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo, Sekta binafsi. |
| | | Mwongozo wa utoaji elimu jumuishi kuhuishwa ifikapo Juni, 2025. | Mwongozo kuhuishwa | 71,000,000.00 | Julai 2024-Juni 2025 | Wizara yenye dhamana ya elimu, Wizara yenye dhamana ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo, Sekta binafsi. |
